



36

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Ruvuma  
Simu Nambari 2602256/2602238  
Fax Na.2602144/2602780  
[rasuvuma@pmoralg.go.tz](mailto:rasuvuma@pmoralg.go.tz)  
[Tovuti: ww.ruvuma.go.tz](http://Tovuti: ww.ruvuma.go.tz)



OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S.L.P. 74,  
**SONGEEA**

Kumb. Na. EA.242/283/01/K/6

15 Julai, 2016

Mkurugenzi Manispaa,  
**Songea.**

*DPEO/TEHAMA*  
*Shirika neni kutekeleza*  
*[Signature]*  
*20/07/2016*

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji,  
**Mbinga.**

Wakurugenzi Watendaji Wilaya,  
**MBINGA, NAMTUMBO, SONGEEA, NYASA,  
TUNDURU, MADABA.**

**YAH: KUTENGA CHUMBA MAALUM CHA MFUMO WA TAKWIMU ZA ELIMU**

Somo la hapo juu linahusika.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI wanatekeleza program ya LANES (Literacy and Numeracy Education Support) katika mikoa 19 ya Tanzania bara, Mkoa wa Ruvuma ukiwa ni mmojawapo.

Ili kutekeleza program hiyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakurugenzi mnaagizwa kutenga chumba maalum cha kuweka mfumo wa Takwimu za Elimu. Chumba hicho kiwe na meza, viti na kiwe na nafasi ya kuweka kompyuta zaidi ya Tatu.

Mnatakiwa kufanya maandalizi haya mapema ili watakapokuja kuweka huo mfumo wakute kipo tayari. Aidha naomba nipate taarifa ya maandishi kuhusu kukamilika kwa maandalizi hayo ifikapo tarehe 29/07/2016.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Kindertu, G.S.A.

Kny: **KATIBU TAWALA MKOA  
RUVUMA**

**Nakala:-** Katibu Tawala Mkoa  
Ruvuma (aione kwenye jalada)